

Kutafuta Mapya

Na Brynn Wengler
Magazeti ya Kanisa

MAHITAJI

- Karatasi ya mstatili kwa ajili ya kila mtu (karatasi ya kawaida iliyokatwa nusu ni nzuri zaidi!)
- Kitu cha kuandikia au kuchorea



Hapa kuna somo la kufurahisha unaloweza kufundisha familia yako au darasa wakati wa mafunzo ya Njoo, Unifuate ya mwezi huu.

UNAPOJARIBU KITU KIPYA, unaweza kujihisi kama Nefi akitafuta bamba za shaba "wala hujui kimbele vitu ambavyo [wewe] ungefanya" (1 Nephi 4:6). Ila kumbuka, hauko peke yako, na hasa kama unafanya kitu ambacho Mungu amaeamuru.

1. Bila ya kujua Kile Kitokeacho

Mpe kila mtu kipande cha karatasi. Ila usiwambie ni cha kazi gani. Badala yake, zungumzia jinsi tunavyopata maono kila mara kutoka kwa Mungu hatua moja kwa wakati (ona 1 Nephi 3-4) au kujenga meli (ona 1 Nephi 17-18).

2. Mstari juu ya Mstari

Sasa inakuja sehemu ya kufurahisha! Soma maelekezo haya kwa sauti moja baada ya mengine kusaidia kundi lako kufumbua fumbo lao kwa ufanuzi. (Ni vigumu, bila picha! Ikiwa watahitaji msaada wa ziada, acha wachukue hatua kwa wakati.)



3. Ufunuo: Kwa kuongozwa na Roho

Familia yako au darasa wanapaswa sasa kuwa na karatasi ambazo zimetengenezwa kuwa boti! Chukua dakika chache kuzungumzia kuhusu nyakati ambapo wote mlihitaji maelekezo ya Mungu mliyohitaji "mstari juu ya mstari." Wangeweza hata kuandikia au kuchora kitu chochote kwenye boti zao kukumbuka nyakati hizo.

Sasa wakati maisha yanaporusha vitu vipyta kwako, usisahau kutafuta ufunuo kutoka kwa Mungu. Kumbuka, daima Ataandaa njia kwa ajili yako kufanya kile Alichokutaka ufanye (ona 1 Nephi 3:7).


MAELEKEZO

1. Shikilia kipande cha karatasi wakati upande mfupi ukiwa juu. Kikunje nusu, juu hadi chini.





2. Kikunje nusu tena kutoka kushoto kwenda kulia, halafu kunjua mkunjo uliotengeneza.

3. Ukiwa na upande uliokunjwa ukitazama juu, chukua kona za juu mbili na uzikunje kwa chini kwenye mkunjo wa katikati. Inapaswa kuonekana kama pembe tatu pamoja na mstatili kwa chini.




4. Shika kipande kidogo cha karatasi kwa chini ya pembe tatu yako na kunja sehemu ya juu. Binua kwa juu na urudie kubinua kwa upande mwininge.




5. Vuta na ufungue kwa sehemu ya chini na sasa inaonekana kama kofia.

6. Endelea kuvuta hadi sehemu za mwisho mbili zikutane na kuwa bapa kama umbo la almasi.



7. Ukiwa na sehemu iliyo wazi kwa chini, kunja sehemu ya kwanza mpaka juu ya umbo la almasi. Binua na rudia kwa upande mwininge. Inatakiwa kuonekana kama pembe tatu.



8. Vuta na fungua sehemu ya chini na ifanye bapa kama uliyofanya kwenye hatua ya 5 na 6 ya umbo la almasi.

